WARAKA WA

# FRATELLI TUTTI

**Wa Baba Mtakatifu Francisko**

Kuhusu Udugu na urafiki kijamii

## NI NINI?

Waraka wa tatu wa Baba Mtakatifu Francisko, baada ya ***Lumen fidei*** (2013) na ***Laudato si*** '(2015).

Ulisainiwa tarehe 3 Oktoba 2020 huko Assisi.

## MISINGI YAKE NI NINI?

- Masuala yanayohusiana na udugu na urafiki kijamii ambayo yamekuwa jambo la kushughulikiwa na Baba Mtakatifu katika miaka ya hivi karibuni.
- Mada zilizowekwa katika Hati juu ya udugu wa kibinadamu kwa ajili ya amani ya ulimwengu na kuishi pamoja uliosainiwa na Iman *Mkuu Ahmad Al-Tayyeb* mnamo Februari 2019.

## UNAMLENGA NANI?

Kwa watu wote ambao wanafanya tafakari hii katika ufunguzi wa mazungumzo.

## JINSI GANI WARAKA UMEGAWANYIKA?

- *Fratelli tutti* inaundwa na utangulizi na sura nane.

**Utangulizi**

**Sura ya 1:** Vivuli vya Ulimwengu uliofungwa

**Sura ya II:** Mgeni katika njia

**Sura ya III:** Kufikiria na kutengeneza ulimwengu ulio wazi

**Sura ya IV:** Moyo uliofunguka kwa ulimwengu wote

**Sura ya V:** Sera bora ya kisiasa

**Sura ya VI:** Mazungumzo na urafiki kijamii

**Sura ya VII:** Njia mpya ya kukutana

**Sura ya VIII:** Dini katika huduma ya udugu ulimwenguni

## UNAPENDEKEZA NINI?

- Ni waraka wa kijamii unaojikita katika udugu na urafiki kijamii.
- Unatazama juu ya mwelekeo wa ulimwengu wa mafundisho kuhusu upendo wa kidugu.
- Unatafakarisha juu ya kutenda na ndoto mpya ya undugu na urafiki kijamii.
- Kuota ndoto moja ya ubinadamu , kama wasafiri walioumbwa na mwili huo huo wa binadamu.

## KICHWA HICHO KINATOKA WAPI?

- *Fratelli tutti* (Wote ni ndugu) ni usemi wa Mtakatifu Fransisko wa Assisi (Admoniciones, 6, 1).
- Mtakatifu aliutumia kupendekeza aina ya maisha na ladha ya Injili.
- Mtakatifu Fransisko alikuwa anawaalika wanaume na wanawake kuwa na upendo unaovuka mipaka ya jiografia na nafasi.

**SALA YA KIKRISTO YA KIEKUMENE**

"Njoo Roho Mtakatifu! Tuonyeshe uzuri wako
Uonekane kwa watu wote wa dunia,
Ili kugundua kuwa kila mtu ni muhimu,
Na kwamba wote ni muhimu, na ni wenye nyuso tofauti
za ubinadamu ule ule uliopendwa na Mungu".
**Amina**

WARAKA WA

# FRATELLI TUTTI


*Wa Baba Mtakatifu Francisko*

Kuhusu Udugu na urafiki kijamii

## VIVULI VYA ULIMWENGU ULIOFUNGWA

*Papa Francisko anaangalia mitindo inayoharibu udugu wa ulimwengu*

**“Jamii inayozidi kuwa ya utandawazi hutuleta karibu, lakini haitufanyi kuwa ndugu”**



### NI VIGEZO GANI VINAVYO DHIHIRISHA VIVULI VYA ULIMWENGU ULIOFUNGWA?

- Ukosefu wa matumaini na kutokuaminiana uliopandwa katika jamii.
- Mivutano ambayo haisaidii mazungumzo na kuishi pamoja.
- Watu ambao wanaonekana “hawafai” na wamebaguliwa.
- Ukosefu wa usawa wa haki na aina mpya za utumwa.
- Kuzorota kwa maadili na kudhoofika kwa maadili ya kiroho.

LEO TUNASHUHUDIA UDANGANYIFU WA MANENO MAKUU:

**UHURU HAKI DEMOKRASIA UMOJA**

MBELE YA HAYA YOTE, *FRATELLI TUTTI* INAONESHA KUWA

**“Njia ni ukaribu na utamaduni wa kukutana”**



Mungu anaendelea kupanda mbegu za mema katika ubinadamu.



Wema, upendo, haki na mshikamano lazima vishindaniwe kila siku.



Tumaini linatazama zaidi ya starehe inayotufunga tusijifungulie mawazo makuu.

WARAKA WA

# FRATELLI TUTTI

Wa Baba Mtakatifu Francisko

Kuhusu Udugu na urafiki kijamii

## MGENI KATIKA NJIA

**NI WAHUSIKA GANI WENGINE KATIKA MFANO WA MSAMARIA MWEMA?**

- MAJAMBAZI
- WALE WANAOPITA MBALI
- MTU ALIYEACHWA NA KUJERUHIWA

**Mbele ya hali hii, *Fratelli tutti* inatuuliza:**

?

Je! Unajitambulisha na nani?
Jirani yako ni nani?



"Yesu hatuiti tujiulize ni akina nani walio karibu nasi, lakini tujifanye kuwa nao".

**_Fratelli tutti_ inashauri ushiriki kikamilifu katika ukarabati wa jamii zilizojeruhiwa.**

LEO HISTORIA YA MSAMARIA MWEMA INAJIRUDIA:

1. Uamuzi au madai yanayo halalisha kutokujali.
2. Jamii inaanza kupoteza hamu ya kujali wengine.
3. Ulimwengu unaruhusu kutengwa.
4. Tunashuhudia kupuuzwa kijamii na kisiasa.

Upendo haujali ikiwa ndugu aliyejeruhiwa anatoka hapa au pale:



**UPENDO HUVUNJA MINYORORO NA HUJENGA MADARAJA.**

**JE! UTAPITA KWA MBALI AU UTASIMAMA MBELE YA MAJERUHI NJIANI?**

Mbele ya maumivu mengi, majeraha mengi, njia pekee ya kutoka ni kuwa kama Msamaria Mwema.

# KUFIKIRI NA KUUNDA ULIMWENGU ULIOFUNGUKA

**Yesu alisema: *"Ninyi nyote ni ndugu"* *(Mt 23: 8)***

## Wito kwa udugu wa ulimwengu unamaanisha uwazi:

- Binadamu hupata utimilifu wake mwenyewe kwa kujitoa kwa wengine.
- Upendo unahitaji uwezo mkubwa wa kukaribisha wengine, ukijumuisha sehemu za pembezoni.
- Upendo ambao unaovuka zaidi mipaka msingi wake ni "urafiki kijamii".



## KUHAMASISHA WEMA MAANA YAKE NI KUHAMASISHA MAADILI AMBAYO HULETA MAENDELEO FUNGAMANI YA BINADAMU.

Je! yanaweza kupatikanaje?

- Kufikiria na kutenda kwa maana ya jumuiya.
- Kupambana na sababu za kimuundo za umaskini na ukosefu wa usawa.
- Kudai serikali iliyopo na hai, ambayo inawekeza kwa jili ya watu dhaifu.
- Kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeachwa.
- Kupata amani ya kudumu kwa kuzingatia maadili ya mshikamano ulimwenguni na huduma.

***Kila mtu ni wa thamani na ana haki ya kuishi kwa hadhi.***

# MOYO ULIOFUNGUKA KATIKA ULIMWENGU WOTE

## JE! NI HATUA GANI ZINAONGOZA UNDUGU WA ULIMWENGU?

**1**

Kukaribisha, kulinda, kuhamasisha na kufungamanisha wahamiaji na wote waliotengwa.

**2**


Kuongeza ufahamu kwamba labda sisi sote tutaokolewa au hakuna mtu anayejikomboa.

**3**

Kutafuta sheria, kisiasa na kiuchumi ulimwenguni ambayo inaleta mshikamano wa watu wote.

## Sifa ya kujitoa bure ni nini?

- Kufanya mambo kwa sababu ndani mwake ni mazuri.
- Kuchukua hatua bila kutegemea kupata matokeo yoyote au chochote cha kubadilishana.
- Kujumuisha wageni wote, na sio wale tu ambao huleta faida zinazoonekana.



"Ubora wa kweli wa nchi mbali mbali za ulimwengu hupimwa na uwezo wa kufikiria pia kama familia ya wanadamu. Mungu daima hutoa bure".

## Kila tamaduni safi kawaida iko wazi na inakaribisha:

Kufungua akili na mioyo yetu hutusaidia kuelewa ni nani tofauti.

Katika umoja wa ulimwengu kila kundi la mwanadamu linapata uzuri wake.

Binadamu ni mtu mwenye mipaka isiyo na kikomo.

Inawezekana kujifungua kwa jirani yako katika familia ya mataifa?

# SERA BORA ZA KISIASA

***"Upendo, kulingana na mafundisho ya Yesu, ndio ufupisho wa Sheria yote"*** *(taz. Mt 22: 36-40)*

## Ni nini maana ya sera nzuri ya kisiasa?

- Imewekwa kwa ajili ya huduma ya wema wa pamoja.
- Siyo tu kutafuta kupata kura.
- Inapendelea njia ya ukuaji wa kibinafsi.
- Huhamasisha uchumi ambao unakuza tofauti za uzalishaji na ubunifu wa ujasiriamali.
- Inafikiria kwa maono mapana na hujumuisha mazungumzo ya kinidhamu.

### *FRATELLI TUTTI* INAALIKA KUWA UTARATIBU WA KIJAMII NA KISIASA AMBAMO ROHO IWE YA UPENDO KIJAMII:

- Inaturuhusu kuendelea kuelekea katika ustaarabu wa upendo ambao sisi sote tumeitwa.
- Inamtambua kila mwanadamu kama kaka au dada, ikijumuisha wote.
- Upendo unahitaji nuru ya ukweli, ambayo pia ni sababu na imani.



**"Upendo kijamii hutufanya tupende wema wa wote na kwa ufanisi hutafuta mema ya watu wote, katika mwelekeo wa kijamii unaowaunganisha".**


**Katika shughuli za kisiasa, kila mtu ni mtakatifu na anastahili upendo wetu na kujitoa kwetu:**

**"Ikiwa unaweza kusaidia mtu mmoja kuishi vizuri, hii tayari inatosha kuhalalisha zawadi ya maisha yako".**

# MAZUNGUMZO NA URAFIKI WA KIJAMII

## "Mazungumzo" yanamaanisha nini?

- **KUKARIBIANA**
- **KUJIELEZA**
- **KUSIKILIZANA**
- **KUTAZAMANA**
- **KUTAMBUANA**
- **KUJARIBU KUELEWANA**
- **KUTAFUTA SEHEMU ZA MAWASILIANO**



### KULINGANA NA UTAMADUNI WA KUKUTANA:

**Inawezekana kujifunza kitu kutoka kwa kila mtu, hakuna asiye na maana, hakuna wa ziada.**

### JAMII YENYE WATU WENGI INAYOALIKA MAZUNGUMZO:

1. Inaheshimu hadhi ya wengine katika kila hali.
2. Inajumuisha hali halisi tofauti, katika kuhakikisha amani ya kweli na thabiti.
3. Inatambua haki ya mwingine kuwa wenyewe binafsi na kumuonesha ukarimu.

### Ni mitazamo au mambo gani ambayo hayasaidii mazungumzo?

- Ushambulizi ambao tunaweza kudhihirisha, kwa mfano, katika mitandao ya kijamii.
- Waongeaji sana ambao hawaachi kusikiliza wengine.
- Kudhihirisha kutokubaliana haraka na kwa njia ya kudhalilisha.

**[ *Mazungumzo halisi kijamii huamua uwezo wa kuheshimu maoni ya mwingine* ]**

# NJIA MPYA YA KUKUTANA


**KATIKA NJIA YA AMANI, MICHAKATO YA UPYAISHO NI MUHIMU SANA:**

- Katika upatanisho wa kweli.
- Katika mpango wa pamoja ambao haumfuti mtu huyo.
- Katika kutambua, kuhakikisha na kujenga upya hadhi ya watu wote.
- Katika upendeleo wa maskini zaidi, wa mwisho, na waliotupwa.
- Katika kurudisha thamani na kuelewa maana ya msamaha.

**Yesu kamwe hakualika watu kushawishi vurugu au kutovumiliana. Injili inatuomba kusamehe *"saba mara sabini"* (Mt 18: 22)**

**MSAMAHA WA KWELI NA UPATANISHO WA KWELI:**

- Unapatikana katika mzozo, kwa kushinda kupitia mazungumzo.
- Unapatikana kwa kujiepusha na vitendo vya uhasama na kuchukiana.
- Unarahisisha majadiliano ya uaminifu, yaliyojengwa juu ya kupenda haki.
- Haumaanishi kusahau au kuadhibiwa.
- Hauanguki kwenye mzunguko mbaya wa kulipiza kisasi.



*"Ninamuomba Mungu aandae mioyo yetu kwa kukutana na ndugu mbali na tofauti za maoni, lugha, tamaduni, dini"*

*PAPA FRANCISKO*

WARAKA WA

# FRATELLI TUTTI

Wa Baba Mtakatifu Francisko

Kuhusu Udugu na urafiki kijamii

## DINI KATIKA HUDUMA YA UDUGU ULIMWENGUNI

### NI KWA KUWA NA DHAMIRI YA WATOTO TU NDIPO MTU ANAWEZA KUISHI KWA AMANI KATI YETU:


| | | |
|---|---|---|
| Dini tofauti hutoa mchango wa thamani kwa ajili ya ujenzi wa udugu. | Kutafuta Mungu hutusaidia kuwatambua wenzetu njiani: **ndugu.** | Kunyimwa uhuru wa dhamiri na dini kunawaacha wanadamu wakiwa maskini. |

### KANISA NI NYUMBA ILIYO NA MILANGO WAZI, KWA SABABU YEYE NI MAMA:

1. Hujenga madaraja
2. Huvunja kuta
3. Hupanda upatanisho

### KATIKA DINI NJIA YA AMANI INAWEZEKANA:

- Sehemu ya kuanzia lazima iwe na mtazamo wa Mungu, kwa sababu Mungu hutazama kwa moyo.
- Ghasia hazina msingi wowote katika imani za kidini.
- Kumwabudu Mungu kwa dhati na unyenyekevu hupelekea heshima maishani, hadhi na uhuru.



> *Viongozi wa dini wameitwa wawe wakweli wa "mazungumzo": kwa kutenda katika ujenzi wa amani kama wapatanishi halisi.*

### SALA YA KIEKUMENE

Mungu wetu, Utatu wa upendo,
kutoka katika muungano wako wa kina kimungu
mimina mto wa upendo wa kindugu kati yetu.
Utupatie upendo uliojitokeza katika ishara za Yesu,
Kwa familia yake ya Nazareti na katika jamuiya ya kwanza ya Kikristo.

Utujalie sisi Wakristo kuiishi Injili
na kumtambua Kristo katika kila mwanadamu,
kwa kumuona akisulubiwa kwa uchungu wa walioachwa
na waliosahaulika katika ulimwengu huu
na kufufuka kwa kila ndugu anayesimama.

Uje, Roho Mtakatifu! Tuoneshe uzuri wako
Unaoonekana katika watu wote wa dunia,
ili kugundua kuwa kila mtu ni muhimu,
na kwamba wote ni wa lazima na ni nyuso tofauti
lakini za ubinadamu huo huo uliopendwa na Mungu.
Amina.